

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA NANE

24 JUNI, 2021



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA NANE – TAREHE 24 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Mwaka 2019/2020.

III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**485. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itasaidia na kufanikisha kutoa Namba kwa Vijiji vya Chipunda, Mkalinda na

Sululu ya Leo vyenye wakazi zaidi ya elfu kumi katika Jimbo la Ndanda.

**486. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Wilaya mpya ya Ukonga katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala.

**487. MHESHIMIWA ALAUDIN HASHAM SALIM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ukosefu wa Dawa na Vifaa tiba katika Vituo vya kutolea huduma za Afya Wilayani Ulanga.

**488. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa mwisho wa mapendekezo ya mgawanyo wa Rasilimali, Madeni, Majengo, Watumishi na Mashamba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

### 489. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

- Je, ni lini Ujenzi wa Barabara ya Magu-Ng'hungumalwa kwa kiwango cha lami utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).

*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
24 JUNI, 2021

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE